
www.vpo.go.tz

OFISI YA MAKAMU WA RAIS

MUUNGANO NA MAZINGIRA TOLEO NO..33 MACHI, 2020

# Mafanikio ya Miaka 56 ya Muungano







Jikinge,

Wakinge na Wengine

**CORONA INAZUILIKA**

# Miaka 56 ya Muungano na mafanikio yake



Tarehe 26 Aprili, 2020 Muungano wetu utatimiza miaka 56 tangu kuasisiwa. Tarehe 26 Aprili, 1964 Mataifa mawili haya ya Jamuhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya watu wa Zanzibar yalioungana na kuunda Taifa jipya la Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ambapo badae ikabadilishwa na kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ni dhahiri kuwa miaka 56 ya Muungano wetu imekuwa yenye kuleta maendeleo kwa Taifa katika Nyanja mbalimbali za kiuchumi, kijamii na kisiasa yanayonufaisha wanachi wa pande zote mbili za Muungano.

Kudumu kwa Muungano huu kumeleta mafanikio makubwa ikiwa ni pamoja na amani na utulivu uliopo nchini mwetu. Wananchi wanafanya shughuli zao za maendeleo kwa uhuru na utulivu sehemu yoyote ya Muungano. Vile vile, wananchi wa pande zote mbili za Muungano wameendelea kuwa na uhusiano na mshikamano wa karibu kadri siku zinavyoendelea. Kadhalika, mwananchi yuko huru kuishi katika sehemu yoyote ya Muungano bila ya bughudha na wananchi wanashirikiana katika kazi za kuendesha maisha yao na kujenga Taifa.

Muungano huu umedumu kutokana na dhamira za dhati za umoja walioku-wanao waasisi wake, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Hayati Shekh Abeid Aman Karume sera sahihi za TANU na ASP na sasa CCM; jitihada zinazoendelezwa na viongozi waliofuatia baada ya waasisi pamoja na kuungwa mkono na wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuthamini manufaa yake. Zaidi ya yote utamaduni wa kukaa na kuzungumzia changamoto zinazojitokeza na kuzifanyia kazi imeongeza ufanisi katika kuufanikisha Muungano wetu.

Katika kipindi cha Miaka 56 ya Muungano, tumeshuhudia mafanikio makubwa ya kujivunia, Watanzania wamejenga umoja na misingi endelevu ya udugu baina yao, ikiwa ni uthibitisho kuwa Muungano unaendelea kuimarika. Kwa kutumia misingi iliyowekwa, wananchi na viongozi wanahakikisha kwamba historia uhuru wa Tanganyika na Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar vinaenziwa. Vile vile, pande mbili za Muungano zimejenga mifumo ya kuendesha Serikali zake kwa uwazi chini ya misingi ya demokrasia na utawala bora. Misingi hiyo imeimarika kutokana na uelewa mzuri wa dhana ya uwajibikaji kwa viongozi wa ngazi zote.

Kipindi chote cha Muungano wetu, tumeshuhudia kuimarika kwa miundombinu ya barabara, usafiri wa anga, usafiri wa majini na kuimarika kwa huduma za jamii. Aidha, tumeendelea kutumia maliasili zetu vizuri zaidi kwa manufaa ya wananchi wa pande mbili za Muungano. Mafanikio hayo yametokana na usikivu, utulivu, uzalendo, moyo wa kujituma na kujitolea na ushirikiano wa dhati wa viongozi na wananchi wote wa pande mbili za Muungano

Tangu Muungano wa Tanganyika na Zanzibar kuasisiwa mwaka 1964, Serikali zetu mbili zimeendelea na jitihada za makusudi za kuhakikisha kuwa masuala yanayoleta vikwazo katika Muungano yanashughulikiwa.

Aidha, Serikali zimeweka utaratibu wa wataalam na viongozi wa kisiasa kukutana na kujadili masuala yanayoonekana kuwa ni changamoto na kutoa ushauri. Pia, utaratibu mwingine ni ule wa kuunda Tume na Kamati ili kuisaidia Serikali katika kushughulikia changamoto hizo.

INAENDELEA UK. 3

# Miaka 56 ya Muungano na mafanikio yake

INATOKA UK. 2

Mafanikio mengine yaliyopatikana katika kipindi cha miaka 56 ni pamoja na: -
Mosi, Sheria nyingi kutungwa au kurekebishwa kwa lengo la kurahisisha utekelezaji wa mambo ya Muungano, kwa mfano:- Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Sheria Na.13 ya 1995; Sheria ya Uhamiaji, Na. 6 ya mwaka 1995 imetungwa na sasa watanzania wanaweza kwenda sehemu yoyote ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bila vikwazo; Sheria ya Mamlaka ya Kodi, Na. 11 ya 1995; Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Na. 1 ya 1995; Sheria ya Tume ya Pamoja na Fedha Na. 14 1996; Sheria ya Biashara ya Bima ya Tanzania Na.18 ya 1996; Sheria ya Usalama wa Taifa Na. 15 ya 1996; Sheria ya Uraia Na. 6 ya mwaka 1995; na Sheria ya Usalama wa Taifa Na. 15 ya mwaka 1995.
Pili, Sheria namba 34 ya mwaka 1994 iliyoanzisha Ofisi ya Makamu wa Rais na kumpatia jukumu lingine la kuratibu ushirikiano katika masuala yasiyo ya Muungano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, lengo ikiwa ni kuimarisha masuala yasiyo ya Muungano ya pande mbili za Muungano;
Tatu, Jeshi la Polisi limefanya kazi kubwa ya kudumisha amani na kushirikiana na wananchi katika shughuli za maendeleo. Jeshi hili limeundwa na askari toka pande mbili za Muungano ambao wanafanya kazi kwa ushirikiano;
Nne, Kuongezeka kwa uelewa kuhusu umuhimu na faida za Muungano kwa umma wa watanzania kuhusu Muungano wetu. Ofisi ya Makamu wa Rais imeendelea na jitihada za kuelimisha umma kuhusu umuhimu na faida za Muungano kupitia Redio, Televisheni, Magazeti, Semina, Warsha, Makongamano, Maonesho ya Kitaifa, Ziara na machapisho;
Tano, Uratibu wa vikao vya kutafutia ufumbuzi changamoto za Muungano. Changamoto



ni: - Utekelezaji wa Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; Utekelezaji wa Merchant Shipping Act katika Jamhuri ya Muungano na Uwezo wa Zanzibar Kujiunga na International Maritime Organisation (IMO); Ushiriki wa Zanzibar katika Jumuiya ya Afrika Mashariki; Uwezo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Kukopa Ndani na Nje ya Nchi; Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT); Ajira kwa Watumishi wa Zanzibar katika Taasisi za Muungano; Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asili; Ongezeko la Gharama za Umeme kutoka TANESCO kwenda ZECO; Ushiriki wa SMZ katika masuala mbalimbali ya Kimataifa na Kikanda; Kuondoa kodi katika unga wa maziwa toka Zanzibar kuja Tanzania Bara; Gharama za Kushusha Mizigo (Landing Fees); na Upatikanaji wa fursa za ushiriki wa Zanzibar katika miradi ya maendeleo ya viwango na ubora wa bidhaa na maendeleo ya wajasiriamali.
Sita, Miradi ya maendeleo imebuniwa na kutekelezwa na Serikali zetu mbili ili kunufaisha wananchi wake. Utekelezaji wake umekuwa na matokeo endelevu katika nyanja zifuatazo: - Elimu; Afya; Masoko; Maji; Mazingira pamoja na Usafiri na Usafirishaji. Miongoni mwa miradi na programu zilizowahi kutekelezwa pande mbili za Muungano na kukamilika ni pamoja na:- Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*Tanzania Social Action Fund -TASAF* ) TASAF I, TASAF II na TASAF III; Programu ya Usimamizi wa Bahari na Environmental Management Programme – MACEMP); Mradi wa Kuongeza Tija na Uzalishaji wa Zao la Mpunga (Expanded Rice Production Project – ERPP); Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabianchi katika Maeneo ya Pwani - LDCF; Mradi wa Udhibiti wa Uvuvi na Maendeleo Shirikishi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi – SWIOFISH; na Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara Tanzania (MKURABITA);
Saba, Uratibu wa masuala ya ushirikiano baina ya Serikali zetu mbili umeendelea kuimarisha Muungano kwani umewekwa Mwongozo wa vikao vya kisekta ambavyo vinasimamiwa na kuratibiwa kwa ushirikiano wa Ofisi ya Makamu wa Rais na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Zanzibar; na
Nane, SMT imejenga majengo kadhaa Zanzibar kwa lengo la kusogeza karibu huduma kwa watanzania wote. Ofisi hizo ni pamoja na: - Ujenzi wa Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais Tunguu, Zanzibar; Ujenzi wa Tawi la Benki Kuu – Gulioni, Zanzibar; Ofisi ya Uhamiaji, Zanzibar; Ofisi ya Bunge Tunguu, Zanzibar; Makao Makuu ya Mamlaka ya Uvuvi katika Ukanda wa Bahari Kuu – Fumba, Zanzibar; na Taasisi ya Sayansi za Bahari –Buyu, Zanzibar. Ofisi zingine zilizoanzishwa ni: - Tume ya Mabadiliko ya Katiba, Kikwajuni - Zanzibar; Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa nchini imefungua Ofisi ndogo - Zanzibar; TANTRADE; NIDA; Sekretarieti ya Ajira, Shangani - Zanzibar; TAEC na COSTECH, Maruhubu – Zanzibar.

**HITIMISHO**

Kimsingi, tunayo kila sababu ya kujivunia kufikisha miaka 56 ya Muungano

INAENDELEA UK.9

# Ofisi ya Makamu wa Rais inavyohamasisha watumishi kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa wa corona

Tanzania ni miongoni mwa nchi duniani zilizoathirika na ugonjwa wa homa kali ya mapafu unaosababishwa na virusi vya corona.

Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kukabiliana na ugonjwa huo ikiweno kuhamasisha taasisi za umma na binafsi pamoja jamii kwa ujumla kuchukua tahdhari ili kujikinga na ugonjwa huo.

Katika kuunga mkono juhudi hizo, Ofisi ya Makamu wa Rais imeendelea kuchukua hatua mbalimbali zikiwemo kutoa elimu kwa watumishi wake kuhusu hatua muhimu za tahadhari zinazopaswa kuzingatiwa. Elimu hiyo inatolewa kupitia semina maalumu, ziara za mara kwa mara za viongozi katika Idara za Ofisi ya Makamu wa Rais na maelekezo ya kujikinga na virusi vya ugonjwa huo katika mbao za matangazo.

Aidha, Ofisi imeweka sabuni na vifaa vya kunawia mikono kila sehemu iliyo wazi, vitakasa mikono (hand sanitizer), kugawa barakoa (masks) kwa watumishi na kuweka msisitizo kwa watumishi wake kuwa na utamaduni wa kujiweka mbali na mikusanyiko (social distance) ili kuepuka maambukizi endapo kutakuwa na mtu mwenye maambukizi.

Pia, watumishi wanasisitizwa kuchukua hatua za haraka za kuwahi kwenye vituo vya afya pindi wanapohisi mafua, homa au shida ya kupumua ili kubaini iwapo wana maambukizi na hatimaye wapatiwe huduma stahiki.

Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais Mhandisi Joseph Malongo ameendelea kuwasisitiza watumishi wake kufuatilia taarifa sahihi kutoka vyombo husika vyenye mamlaka kama vile Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.




*Sehemu ya Watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo Mhandisi Joseph Malongo wakimsikiliza Bw. Yusuph Seif Afisa Afya kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamiii, Jinsia, Wazee na Watoto alipokuwa akitoa elimu juu ya ugonjwa wa Corona ofisni hapo Mtumba jijini Dodoma.*

# Ukuta wa Pangani mkombozi wa wananchi



*Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa akikagua mradi wa ujenzi wa ukuta wa mto Pangani kabla ya kuzindua ukuta huo. Kushoto ni Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mhe Mussa Sima na kulia ni Mkuu wa wilaya ya Pangani, Zainab Abdallah Issa.*

Serikali ya Tanzania kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais inaendelea kutekeleza miradi mbalimbali katika kuhakikisha suala zima la uhifadhi wa mazingira linasimamiwa ipasavyo.

Miongoni mwa mambo yanayochangia uharibifu wa mazingira ni changamoto ya mabadiliko ya tabianchi hivyo Serikali imewezesha Mradi wa ujenzi wa ukuta wa Pangani upande wa kaskazini mwa nchi ili kukabiliana na changamoto hiyo.

Machi 6, 2020 Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa aliweka Jiwe la Msingi na kuzindua ujenzi wa ukuta wa Pangani wilayani Pangani mkoani Tanga.

Mradi huu umejenga ukuta wenye urefu wa mita 950 ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mradi wa Kujenga Uwezo Kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabianchi yanayotokana na kuongezeka kwa ujazo wa bahari katika maeneo ya Pwani ya Bahari ya Hindi.

**Manufaa ya mradi**

Mradi wa ujenzi wa ukuta wa mto Pangani na upandaji mikoko umeleta manufaa kwa wananchi wa Pangani ikiwemo kutoa ajira kwa zaidi ya watu 200, kusaidia kukinga mji wa Pangani upande wa kaskazini na athari za kuongezeka kwa ujazo wa bahari na mawimbi.

Aidha, ujenzi wa ukuta huu, umeleta mandhari nzuri ya kupumzikia na eneo hilo linaweza kutumiwa na Halmashauri kama chanzo cha mapato. Pia, mikoko iliyopandwa itaongeza mazalia ya samaki na viumbe wengine wa baharini.

Mradi wa Ujenzi wa Ukuta wa Pangani umesimamiwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Miradi kwa kushirikiana na Shirika la Mazingira Duniani (UNEP) na kuratibiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya hiyo.

Hivyo mradi huu ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi wa mwaka 2007 na Mkakati wa Taifa wa Mabadiliko ya Tabianchi wa mwaka 2012.

**Kazi zilizofanyika**

Kazi zilizofanyika katika mradi huu ni upandaji miti ya mikoko mbele ya ukuta uliojengwa na pembeni mwa mto Pangani, ujenzi wa ukuta wa zege kipande cha urefu wa mita 950, uwekaji wa vyuma vya usalama kwenye ukuta, ujenzi wa eneo la kutembelea na ujenzi wa mitaro ya maji ya mvua.

INAENDELEA UK. 9

# Sh. Bilioni 1.2 zanufaisha wilaya za Mwanga, Same

Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais imekuwa ikitekeleza miradi mbalimbali kwa lengo la kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi katika maeneo tofauti hapa nchini.

Miongoni mwa miradi hiyo ni mradi wa kujenga uwezo wa Taasisi na Jamii katika kuhimili athari hizo kwenye maeneo ya kaskazini mwa nchi unaotekelezwa katika wilaya za Mwanga na Same (Kilimanjaro).

**Umuhimu wa mradi**

Mradi huu unasaidia kuimarisha ukusanyaji, uchakataji na upatikanaji wa taarifa sahihi za hali ya hewa kwa maeneo ya Same na Mwanga na hatimaye taarifa hizi kutumika katika kupanga mipango ya kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi katika wilaya hizi.

Miongoni mwa mafanikio ya mradi huu ni ununuzi wa mitambo miwili ya utabiri wa Hali ya Hewa katika kila Wilaya. Hii itasaidia Serikali na jamii nzima kuwa na mipango thabiti ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ikiwemo ukame na mafuriko.

Aidha, mradi huu utaimarisha miundombinu ya umwagiliaji kwa kukarabati mfereji mkuu wa umwagiliaji katika kijiji cha Mabilioni wilayani Same wenye urefu wa km 1.8 kwa kuujenga upya na kuusakafikia *(lining).*

Awali mfereji huu ulikuwa umejengwa kienyeji na hivyo kupoteza maji mengi. Kwa ukarabati huu, maji mengi yatatiririka kuelekea mashambani na hivyo kuongeza eneo la umwagiliaji kutoka hekta 400 za sasa mpaka kufikia takriban hekta 1,200.

Aidha kupitia ukarabati utakaofanyika chini ya ufadhili wa mradi huu kiwango cha uzalishaji wa mpunga kitaongezeka kutoka kilo 700 kwa hekta (kwa sasa) hadi kilo 2000 kwa hekta.



*Sehemu ya mfereji mkuu wa umwagiliaji katika Kijiji cha Mabilioni wilayani Same mkoani Kilimanjaro ambao umejengwa na kusakiafiwa (lining) ambao hapo awali ulikuwa umejengwa kienyeji.*

Ni dhahiri utekelezaji wa Mradi huu katika kijiji cha Mabilioni utaleta mapinduzi makubwa kwa kuongeza tija kwenye kilimo na hivyo kuongeza uwezo wananchi katika eneo hili kwa kuzalisha zaidi na kujitosheleza kwa chakula.

Katika kuimarisha miundombinu kwa ajili ya upatikanaji wa maji safi na salama Wilayani Mwanga, Mradi utajenga miundombinu ya upatikanaji wa maji safi na salama kwenye vijiji vya Jipe na Makuyuni.

Upatikanaji wa uhakika wa maji safi na salama katika vijiji hivi umekuwa ni changamoto kubwa kutokana na hali ya ukame iliyokithiri katika maeneo haya ikichangiwa na mabadiliko ya tabianchi.

Utekelezaji wa Mradi huu katika vijiji hivi utasaidia kuleta nafuu mkubwa wa maisha katika jamii kwani takriban watu 5000 wataweza kupata uhakika wa maji safi na salama.

Aidha upatikanaji wa maji safi na salama utapunguza kwa kiasi kikubwa magonjwa yatokanayo na maji yasiyo salama na hivyo sehemu kubwa ya kipato cha

INAENDELEA UK.9

# Ijue Tuzo ya Rais ya Kuhifadhi Mazingira



Tuzo ya Rais ya Kuhifadhi Mazingira hutolewa kwa lengo la kuchochea na kutoa hamasa kwa jamii kushiriki katika hifadhi ya mazingira ili kukabiliana na uharibifu wa mazingira, hususan katika ardhi, misitu, vyanzo vya maji na uchafuzi wa hewa.

Tuzo hii inahusisha watu binafsi, vikundi vya kijamii, mashirika na makampuni ya umma na binafsi, taasisi za umma na binafsi, asasi zisizo za kiserikali, Shule Vyuo na taasisi za elimu na utafiti na mamlaka za serikali za mitaa.

Tuzo ya Rais ya Kuhifadhi Mazingira imeboreshwa kwa kujumuisha masuala yote yanayohusu hifadhi na usimamizi wa mazingira ukilinganisha na tuzo ya awali iliyoendeshwa kwa kipindi cha 2010-2018 ambayo ilijikita katika kuhamasisha hifadhi ya vyanzo vya maji, Kupanda na kutunza miti tu. Tuzo ya awali ilijulikana kamaTuzo ya Rais ya Kuhifadhi Vyanzo vya Maji Kupanda na Kutunza Miti.

Mikoa iliyotoa washindi wa Tuzo ya awali (2010 – 2018) ni pamoja na mkoa wa Morogoro, Iringa, Mwanza, Shinyanga, Simiyu, Tanga, Lindi, Mtwara, Kagera, Kilimanjaro, Tanga Ruvuma na Pwani. Baadhi ya shughuli zilizopatiwa tuzo ni pamoja na kuhifadhi vyanzo vya maji na kuvuna maji ya mvua, kupanda na kutunza miti, kutumia nishati mbadala, kutumia mbolea ya samadi kwenye shughuli za kilimo, kuweka usimamizi mzuri wa utupaji wa taka aina zote, kufuga mifugo kwa njia endelevu pamoja na kutumia majiko banifu.

Uwepo wa Tuzo umechagiza ushiriki wa wananchi katika kuhifadhi mazingira hivyo kuboresha hali ya mazingira nchini. Aidha, sehemu kubwa ya jamii inafanya shughuli za kuhifadhi mazingira kama njia ya kujiongezea kipato hivyo kudhihirisha umuhimu wa hifadhi ya mazingira kwa ajili ya maendeleo endelevu.



## ZIARA YA KAMATI YA BUNGE

# Zungu:Miradi ya SGR na Kinyerezi imekidhi viwango vya mazingira

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Mussa Azzan Zungu amesema kuwa mradi wa reli ya kisasa (SGR) na mradi wa kuzalisha umeme kwa gesi wa Kinyerezi imezingatia vigezo vya mazingira.

Zungu alisema hayo jana wakati akiwasilisha taarifa mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira Mhe. Sadiq Murad ilipotembelea na kukagua miradi hiyo jijini Dar es Salaam.

Akiipongeza miradi hiyo alibainisha kuwa kama Ofisi ya Makamu wa Rais wameshirikishwa katika hatua zote za utekelezaji wa mradi tangu kuanza kwake hadi unavyoendelea.

"Tumekuja hapa na tumejiridhisha mradi huu umefuata taratibu zote za mazingira na vibali vyote vilitolewa pamoja na mapendekezo ya maeneo ya kufanyia maboresho, NEMC (Baraza la taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira) walikuja hapa Kinyerezi mara tano kuthibitisha, taka ngumu na za sumu zinadhibitiwa na pia misitu yetu ipo salama," alisema Zungu.

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira imepongeza Serikali kwa utekelezaji wa miradi ya reli ya kisasa (SGR) na ule wa kuzalisha umeme wa Kinyerezi jijini Dar es Salaam.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Mwenyekiti hiyo Sadiq Murad wakati wa ziara ya kutembelea na kukagua uzingatiaji wa sheria ya mazingira katika miradi hiyo.

Alisema mradi wa SGR unaotekelezwa na Serikali kupitia Shirika la Reli Tanzania (TRC) pamoja na kuwa unakwenda kwa kasi kuelekea kukamilika lakini pia umekidhi vigezo vyote vya mazingira.

Aidha mwenyekiti huyo aliagiza Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kuendelea kusimamia kwa karibu masuala yote yanayohusu mazingira katika miradi hiyo ili kuepuke athari zinazoweza kujitokeza kwa jamii na mazingira hapo baadae.

Niwapongeze mkurugenzi wa TRC na timu yake kwa kweli wamejitahidi sana kwa ujenzi huu na unakwenda kwa spidi nzuri lakini NEMC wana kazi ya ziada ya kuendelea kuwa karibu nao waje kuwashauri kwani ushauri wao utakuwa na faida kubwa kwa nchi yetu hapo baadae," alisisitiza Murad.

Kwa upande wake Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani alisema katika miradi hii Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kila mwaka wanatenga sh. milioni 50 kwa ajili ya utunzaji wa mazingira.





## Ukuta wa Pangani mkombozi wa wananchi

INATOKA UK.5

Pia kazi zingine ni ujenzi wa mabenchi ya kupumzikia seti 10, ufungaji wa taa 12 za sola pembeni ya ukuta, ujenzi wa choo cha umma chenye matundu 8, na uwekaji mawe mbele ya ukuta uliojengwa ili kupunguza kasi ya mawimbi ya bahari.

**Usimamizi wa baadae na uendelevu wa mradi**

Mradi utakabidhiwa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Pangani ili iendelee kuusimamia na kuutunza ikiwa ni pamoja na utunzaji wa miti ya mikoko iliyopandwa mbele ya ukuta.

**Hatua zinazoendelea kuchukuliwa**

Hatua zinazoendelea kuchukuliwa ni kuelimisha umma kuhusu mabadiliko ya tabianchi, kuhamasisha upandaji wa miti ya mikoko pembeni ya mto na kuendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kujenga miundombinu ya kukinga maeneo mengine yaliyo katika hatari ya kuathirika.

Mradi huu umetekelezwa katika kipindi cha mwaka 2016 hadi 2019 na kugharamiwa na Mfuko wa Nchi Maskini Duniani ulioko chini ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi kwa kwa kushirikiana na Serikali ya Tanzania na umegharimu kiasi cha Dola za Marekani 1,294,698.79.




*Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akizindua mradi wa ujenzi wa ukuta wa mto Pangani mkoani Tanga. Wa pili kulia ni Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mussa Sima.*

INATOKA UK..3

wa Tanganyika na Zanzibar. Zipo sababu nyingi za kujivunia zikiwemo Muungano wetu kudumu kwa muda mrefu. Ifikapo tarehe 26 Aprili 2020, Muungano wetu utakuwa umedumu kwa miaka 56 sasa na Kauli Mbiu ya mwaka huu ni: **'MAENDELEO YA TANZANIA KIUCHUMI YANATEGEMEA MUUNGANO IMARA, SIASA SAFI NA UONGOZI BORA, TUMIA KURA YAKO KUCHAGUA VIONGOZI BORA 2020''.** Bila shaka ni wajibu na jukumu la kila Mtanzania kuulinda, kuimarisha na kuudumisha Muungano wetu kwa kwa maendeleo endelevu ya taifa letu.

## Bilioni 1.2/= zanufaisha wilaya za Mwanga, Same

INATOKA UK.4

familia itatumika zaidi katika shughuli za maendeleo badala ya kutibu magonjwa haya.

**Shughuli zilizotekelezwa hadi sasa**

Shughuli zilizotekelezwa katika kipindi hiki ni pamoja na ukarabati wa mita 1,800 za mfereji wa umwagiliaji katika kijiji cha Mabilioni (Same) unaendelea na mafunzo kwa wanakijiji 30 kuhusu kilimo endelevu cha umwagiliaji katika kijiji cha Mabilioni (Same) yamefanyika.

Pia yametolewa mafunzo kwa wanakijiji 30 kuhusu matumizi endelevu ya maji katika vijiji vya Jipe, Makuyuni na Kambi ya Simba sambamba na kuandaliwa kwa kwa Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini wa utekelezaji wa mradi. Aidha kwa upande mwingine Kikao cha kamati ya Usimamizi wa Mradi (*Steering Committee Meeting*) kimefanyika.

**Gharama**

Mradi huu wa miaka miwili unatekelezwa kwa gharama ya Euro 469,000 na kusimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na Halmashauri husika pamoja na wataalamu wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (African Development Bank – AfDB).

# NEMC yahimiza matumizi ya mifuko ya karatasi



Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Dkt. Samuel Gwamaka amewataka Watanzania kuanza kutumia mifuko mbadala ya karatasi kwani haina athari kiafya pia ni rafiki kwa mazingira.

" Ni jambo la kushangaza kuona asilimia kubwa ya mifuko ya karatasi inayotumika nchini Rwanda na Kenya inazalishwa Tanzania huku watanzania bado wakiendelea kutumia mifuko ya plastiki ambayo imeshazuiliwa. jambo linalokinzana na dhana ya kukuza uchumi wa viwanda,'' alisema Dkt Gwamaka.

Akizungumza katika ziara yake ya siku moja kutembelea Kiwanda cha karatasi cha Mufindi paper Mills ltd (MPM), kilichopo Wilayani Mufindi katika mkoa wa Iringa kujionea uwezo wa kiwanda kuzalisha malighafi kwa ajili ya bidhaa mbadala za mifuko ya kubebea pamoja na vifungashio, Dkt. Gwamaka alipongeza kiwango cha bidhaa zinazozalishwa na kiwanda hicho kwa sasa.

Alisema toka wapige marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki mwaka jana kumekuwa na tofauti kubwa kwani matumizi ya bidhaa hiyo yameongezeka kwa kiasi kikubwa kutokana na takwimu za uzalishaji zilizopo viwandani.

"Awali kiwanda cha Mufindi paper Mills ltd (MPM), Mwaka 2014,2015 kilikuwa kinauza tani 15,000 kwa soko la ndani ambapo kwa nje ilikuwa tani 26,000," alisema Dkt. Dkt. Gwamaka na kuongeza kuwa kinachoshangaza kuwa kwa mwaka jana 2018/2019 uzalishaji umepungua mpaka kufikia tani 7,000 kwa soko la ndani wakati soko la nje ulipanda mpaka kufikia tani 40,000.

Dkt. Gwamaka alisema kuna baadhi ya wafanyabiashara ambao siyo waminifu wameendelea kuingiza nchini mifuko ya plastiki kupitia njia za panya, hali inayochangia ongezeko la mifuko sokoni na kusababisha kufa kwa viwanda vya ndani na hatimaye kukosa mapato ya Serikali.

" Kuna baadhi ya Wafanyabiashara wamekuwa wakiingiza au kuzalisha mifuko ambayo haina nembo za mzalishaji, nembo ya shirika la viwango hapa nchini (TBS) pamoja na ubora wa GSM 70, hivyo inatulazimu kuchukua hatua kali ili kulinda viwanda vya ndani ambavyo bidhaa zake zimekuwa zikipata ushindani,'' alisema Dkt. Gwamaka.

Dkt Gwamaka alisema kwa mujibu wa Sheria mpya ya mazingira watu ambao watazalisha au kuingiza nchini mifuko hiyo batili, hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao ikiwemo faini kubwa.

"Wakati umefika kwa watanzania kuachana na tabia ya kulalamika suala la ajira badala yake kuanza kuchangamkia fursa zinazojitokeza kupitia rasilimali misitu ambapo kuna fursa nyingi za kujikwamua kiuchumi hali itakayofanikisha kufikiwa kwa azma ya serikali ya ujenzi wa uchumi wa kati na viwanda ifikapo mwaka 2025,'' alisisitiza huko akiwaomba watanzania kutumia mifuko ya karatasi.

Kwa upande wake Kaimu Meneja Mkuu wa kiwanda hicho, Mwandisi Gregory Chogo alisema wakati umefika watanzania kuchangamkia fursa kupitia bidhaa mbadala za mifuko ya kubebea pamoja na vifungashio vinavyotokana na karatasi.

Alisema kiwanda kinatambua mchango wa wajasiliamali wadogo na hivyo kimeamua kuwatengea vifurushi vya kuuza kuanzaia kilo 100 na lengo likiwa kutokomeza matumizi ya mifuko ya plastiki hapa nchini.

Tangu katazo la uzalishaji, usambazaji na matumizi ya mifuko ya plastiki juni mwaka jana, NEMC imekuwa ikitoa elimu kwa umma na pia kutembelea maeneo mbalimbali hapa nchini kuhusu umuhimu wa matumizi ya mifuko na vifungashio mbadala kwa usalama wa mazingira na afya za watu.

# Zungu aonya wachimbaji wanaokiuka sheria

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Mussa Azzan Zungu amewaonya wachimbaji wadogo wa dhahabu wanaokiuka sheria ya mazingira kwa kushindwa kudhibiti kemikali ya zebaki na kutiririka ovyo.

Zungu alitoa onyo hilo jana wakati wa ziara yake ya kikazi wilayani Butiama mkoani Mara alipotembelea maeneo ya wachimbaji wadogo Sirori Simba na Buhemba.

Katika ziara hiyo ambayo pia aliitumia kusikiliza kero za wachimbaji hao wadogo na kuangalia uzingatiaji wa sheria ya mazingira yam waka 2004, waziri huyo alibainisha kuwa kemikali ya zebaki ina madhara kwa afya na mazingira.

Alisema kwa sasa bado haujapatikana mbadala wa kemikali hiyo lakini ni wajibu wa wachimbaji hao kuitumia kwa uangalifu ili kuhakikisha haisambai ovyo na kusababisha uchafuzi wa hasa kwenye vyanzo vya

"Elimu iendelee kutolewa kuhusu madhara ya kutotumia zebaki kwa uangalifu na hali kama hii itawafanya wananchi wetu waugue na wakiugua Serikali inaingia gharama ya kuwatibu maradhi yanayotokana na udhaifu wa kushindwa kusimamia mazingira vizuri," alisema Zungu.

Aidha katika kukabiliana na uharibifu wa mazingira unaosababisha changamoto ya mabadiliko ya tabianchia aliwaonya kuacha kukata miti wanayotumia kuimarisha kuta za mashimo na badala yake watumie njia nyingine mbadala.

Waziri huyo aliwataka wachimbaji wadogo kupanda miti ma wanavyofanya wa ajili ya kuitumia katika migodi na kusema kuwa huo ni uharibifu wa mazingira hivyo akawataka wapande miti kwa wingi ili kuhifadhi mazingira.

"Ndugu zangu wachimbaji wadogo Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli ameanzisha masoko ya madini na nyie munge mkono kwa kuhifadhi mazingira, mpande miti kwa wingi," alisisitiza.

Katika hatua nyingine Waziri Zungu ameliagiza Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kupitia ofisi zake za kanda kuacha mara moja utaratibu wa kuwatoza wachimbaji wadogo bila kuwapa elimu.

Akiwasilisha malalamiko hayo mbele ya waziri, Mwenyekiti wa Wachimbaji wadogo mkoa wa Mara, John Liyamera aliiomba Serikali kupitia maafisa mazingira wawe wanawatembelea wachimbaji kuwapa elimu.

Alidai wachimbaji hao wako tayari kulipa tozo ili kuongeza mapato ya Serikali lakini kinachowakwamisha ni kuwa hawapati elimu kuhusu uhifadhi wa mazingira.



***Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Mussa Azzan Zungu akiangalia namna mabaki ya zebaki yanavyotiririka katika maeneo ya machimbo ya wachimbaji wadogo ya Sirori Simba wilayani Butiama mkoani Mara alipofanya ziara.***

# Sima awataka wananchi kulinda miti inayopandwa



*Sehemu ya mikoko iliyopandwa katika Delta ya Mto Rufiji wilayani Kibiti mkoani Pwani kupitia Mradi wa LDCF ambayo imepandwa kuhimili changamoto ardhi kuliwa na mto.*

Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Mussa Sima (pichani chini) ametoa mwito kwa wananchi kulinda miti inayopandwa ili kusaidia kuhifadhi mazingira.

Sima alitoa mwito huo wakati alipotembelea maendeleo ya miti ya mikoko iliyopandwa katika Delta ya Mto Rufiji kupitia mradi wa LDCF ambayo ilipandwa kwa lengo la kuhimili changamoto ardhi kuliwa na mto.

Alisema kuwa Ofisi ya Makamu wa Rais kama mratibu wa mradi huo imefika mikoko iliyopandwa katika eneo la Kikale wilayani Kibiti mkoani Pwani.

"Kama Serikali tunammepanda mikoko na nawaopanda ba muendelee kuilinda miti hii na mtoe taarifa kama kuna vitendo vya ukataji vinafanyika hivyo
muwe sehemu ya kulinda," alisisitiza.

Naibu waziri huyo awali akizungumza ofisini kwa Mkuu wa wilaya ya Kibiti alibainisha kuwa lengo la mradi huo pia lilikuwa ni kutoa elimu kwa wananchi ku-



Alisema kuwa ni matumaini ya Serikali kuona mara baada ya mradi huo.
wananchi wanaozunguka eneo la mradi wanaacha kukata miti kwa ajili ya mkaa, mbao au kufanya kilimo holela kwenye delta hiyo.

"Watu wengi wamezoea mradi ukiisha basi sasa Serikali inafuatilia miradi yote kuona impact yake leo mmomonyoko ukijitokeza
unaongeza ujazo wa maji yam to na kusababisha mabadiiko ya tabianchi.

Mpango wa usimamizi shirikishi katika maeneo yalipopandwa mikoko umekamilika kwa vijiji vine vya mfradi huo ambavyo ni Mfisini, Mchinga, Nyamisati na Kikale.

Aidha eneo la ekari 208 limepandwa mikoko ambayo imeota ambapo pia urudishaji wa miti hiyo katika eneo lenye ukubwa wa ekari 792 umefanyika.

# Habari katika picha



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais- Muungano na Mazingira Mh. Mussa Zungu akielezea jambo wakati wa ziara ya kutembelea kijiji cha Kwamgogo kilichoko kisiwani Pemba ambapo alienda kujionea athari za kimazingira katika kijiji hiko ambazo zimesababishwa na mabadiliko ya tabianchi.*



*Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Mussa Sima akiwa katika ziara ya kukagua mradi wa upandaji mikoko katika Delta ya Mto Rufiji wilayani Kibiti mkoani Pwani ambao ni sehemu ya utekelezaji wa Mradi* wa ***Kujenga Uwezo Kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabianchi katika maeneo ya Pwani ya Bahari ya Hindi.***



# Waziri Zungu:Serikali kupanua wigo wa kutekeleza miradi ya maendeleo

Serikali itaendelea kutoa kipaumbele katika kutafuta rasilimali fedha za ndani na nje ili kupanua wigo wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kuboresha uhifadhi na usimamizi wa mazingira nchini.
Kauli hii imetolewa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Mussa Zungu hii leo jijini Dodoma mara baada ya kuwasilisha taarifa ya Ofisi yake kuhusu utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa na Ofisi hiyo.
Amesema miradi katika Ofisi yake imechangia kwa kiasi kikubwa katika kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi; kupunguza uharibifu wa mazingira, kuongeza usalama wa chakula na kuboresha hali ya uchumi kwa jamii; kupunguza uchafuzi wa mazingira na kulinda afya ya jamii.
"Umuhimu wa kuhifadhi mazingira unatokana na ukweli kwamba matumizi ya rasilimali za mazingira ndio msingi mkuu wa ukuaji wa uchumi wa nchi pamoja na maendeleo ya Taifa na jitihada za kuondoa umasikini nchini zinaendana na matumizi endelevu ya rasilimali za mazingira" Zungu alisisitiza.

Amesema changamoto za uharibifu wa Mazingira nchini ni kubwa na kutolea mfano kukithiri kwa matumizi ya kuni na mkaa na athari za mabadiliko ya Tabianchi.
Ameainisha kuwa ofisi yake imedhamiria kupunguza uharibifu wa mazingira nchini kwa kuhamasisha matumizi ya nishati mbadala. "Nimeongea na kampuni za usambazaji wa nishati ya gesi hapa nchini ili kupunguza gharama za nishati hili ili kila mwananchi aweze kunufaika nayo na kwa kuanzia kampuni ya Kopa gesi wamekuja na teknolojia ya kuuza gesi kwa reja reja"
Akitoa ufafanuzi juu ya kukithiri kwa magugu maji katika Ziwa Victoria, Waziri Zungu amesema Serikali inaangalia namna bora ya kuvuna magugu maji hayo ili kunusuru viumbe hai na bioanuai inayopatikana katika maeneo hayo.
Kwa upande mwingine Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda Biashara na Mazingira Mhe. Murad Sadiq ameishauri Serikali kuweka mkazo katika usimamizi wa Serikali hususan udhibiti wa kelele katika makazi ya watu.

Aidha, Mjumbe wa Kamati hiyo Hawa Mwaifunga ameshauri Serikali kuendelea kutoa elimu ya athari za matumizi ya Zebaki kwa wachimbaji wadogo hapa nchini.
Suala la uhifadhi na usimamizi wa mazingira ni mtambuka, hivyo utekelezaji wake unahusisha sekta zote na jamii kwa ujumla. Hivyo, Ofisi ya Makamu wa Rais inaratibu utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambayo ni muhimu katika kutatua changamoto za mazingira na ustawi wa jamii ambapo katika mwaka 2019/20 ilipanga kutekeleza jumla ya miradi mitano (5) ya maendeleo.
Miradi hiyo ni pamoja na Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Ardhi ya Bonde la Ziwa Nyasa; Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kutekeleza Mkataba wa Montreal Kuhusu Udhibiti wa Kemikali Zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni; na Mradi wa Kutekeleza Mpango wa Kitaifa wa Utekelezaji wa Mkataba wa Stockholm unaohusu Kemikali zinazodumu katika Mazingira kwa Muda Mrefu.
Miradi mingine ni pamoja na Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi kupitia Mifumo ya Ikolojia; na Mradi wa Kusaidia Kujenga Uwezo wa Taasisi na Jamii Kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabianchi Kwenye Maeneo ya Kaskazini mwa Nchi.

Jikinge,

Wakinge na Wengine

**CORONA INAZUILIKA**

# Serikali inavyosimamia kemikali, taka hatarishi

Imebainika kuwa wafanyakazi wa sekta za kilimo na viwanda wako hatarini zaidi kupata madhara yatokanayo na matumizi ya viuatilifu hatarishi na kemikali za viwandani lakini nchi inakabiliwa na changamoto ya uwezo mdogo wa ufuatiliaji wa matumizi ya kemikali hizo katika mazingira.

Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazoendelea ambazo zinaathiriwa na ongezeko la changamoto hiyo katika usimamizi wa kemikali na taka hatarishi ikiwemo uelewa mdogo wa jamii juu ya madhara ya kemikali na taka hatarishi.

Changamoto hizo zinatokana na idadi kubwa ya watu kuwa na uelewa mdogo kuhusu madhara yatokanayo na kemikali.

Vilevile, sekta ya mafuta na gesi hutegemea matumizi ya kemikali mbalimbali ambazo zinahitaji usimamizi endelevu ili kuepuka madhara yatokanayo na kemikeli na taka hatarishi.

Kwa muktadha huo, Ofisi imeandaa Mkakati wa usimamizi na udhibiti wa kemikali na taka hatarishi utakaotekelezwwa kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia 2020 hadi 2025.

**Malengo ya mkakati**

Mkakati huu unalenga kutoa mwongozo wa kitaifa na kuboresha uratibu na usimamizi endelevu wa hatua za kimkakati kwa kila mtu, ngazi za mitaa na kitaifa katika kukuza usimamizi jumuishi wa kemikali na taka hatarishi.

Aidha mkakati huu unawezesha usimamizi na udhibiti wa athari zitokanazo na kemikali, kuimarisha mfumo wa usimamizi wa elimu, uhamasishaji wa umma na uelewa kuhusu kemikali na taka hatarishi na kuwezesha mfumo wa kitaasisi, Sera na Sheria katika usimamizi bora wa kemikali na taka hatarishi.

Pia kuongeza ushirikiano wa kitaalamu na ufanisi katika kuhamasisha usimamizi bora wa kemikali na taka hatarishi, kuandaa na kutekeleza mifumo ya kubaini, kuzuia na kutoruhusu usafirishaji haramu wa kemikali na taka hatarishi.

Malengo mengine ni kuwezesha utupaji salama wa kemikali zilizokwisha muda wa matumizi na vibebeo vilivyotumika na Kutoa mafunzo kwa watumiaji na wafanyabiashara kuhusu usimamizi sahihi wa kemikali zilizokwisha muda wa matumizi na vibebeo vilivyotumika.

**Changamoto za usimamizi wa kemikali na taka hatarishi**

Hali halisi ya udhibiti na usimamizi wa kemikali na taka hatarishi nchini inaonesha uwepo wa changamoto kadhaa ambazo ni pamoja na uhaba wa miundombinu ya uteketezaji wa kemikali na taka hatarishi, uwezo mdogo wa kitalaam na kitaasisi katika kudhibiti na kusimamia kemikali na taka hatarishi.

Changamoto zingine ni mifumo duni ya uratibu katika Sekta kuhusu udhibiti na usimamizi wa kemikali, uhaba wa Rasilimali fedha; Uhaba na ukosefu wa Takwimu kuhusu udhibiti na usimamizi wa kemikali



taka hatarishi, ushiriki mdogo wa wadau muhimu hususani NGO na sekta binafsi.

Pia kutokuwa na Programu za kutosha za kubadilishana taarifa kati ya nchi na nchi, kuhusu Mbinu bora na rafiki kwa mazingira zinazohusiana na udhibiti na usimamizi wa kemikali na Taka, ukosefu wa teknolojia rahisi na kemikali mbadala, ukosefu wa mipango ya pamoja katika kutekeleza ajenda za kemikali na shughuli zilizopo chini ya mikataba ya kimataifa, kutokuwa na uchambuzi wa kutosha wa faida na hasara kuhusu udhibiti na usimamizi bora wa kemikali na taka na Usimamizi mdogo wa sheria zinazohusu udhibiti wa kemikali na taka hatarishi.

**Masuala mapya yanayojitokeza katika usimamizi wa kemikali na taka hatarishi**

Mkakati huu umegusa masuala mapya yanayoibuka kama changamoto kwenye mazingira. Aidha, tafiti za kisayansi zinaonesha uwepo wa masuala mapya yanayoibuka katika sekta ya mazingira kutokana na kemikali na taka hatarishi.

Masuala hayo ni pamoja na

*Mosi;Bidhaa zenye viambata vya Kemikali*

Bidhaa zenye viambata vya kemikali zinajumuisha dutu au sumu ambazo huingizwa kwenye bidhaa na huhatarisha afya ya binadamu na mazingira. Baadhi ya wazalishaji wa bidhaa zenye viambata vya kemikali hatari hawatoi taarifa juu ya madhara yatokanayo na viambata vya kemikali vilivyomo kwenye bidhaa hizo.

*Pili;Nanoteknolojia na bidhaa zitokanazo na Nanoteknolojia*

Nanoteknolojia ni sayansi ya kubadili na kutumia maunzi au maada katika kipimo kidogo sana (nanomita 1-100) ambapo huwa na tabia mpya, bora na za kipekee za kimaumbile, kikemia au kibailojia zinazosaidia katika uzalishaji wa vifaa vyepesi vilivyo imara zaidi; vyenye uwezo mkubwa wa kupitisha joto au umeme; au vyenye kiwango kikubwa cha mmenyuko wa kikemikali.

*Tatu;Dutu Hatarishi katika muda wa matumizi ya Vifaa vya Umeme na Kielektroniki*

Matumizi ya vifaa vya umeme na kielektroniki unaongezeka na kusababisha kuongezeka kwa kasi kwa taka za kielektroniki katika mazingira. Madhara ya taka za kielektroniki yanatokana na kemikali hatarishi zilizomo katika vifaa kama vile risasi, cadmium, chromium. na polychlorinated (PCBs).

*Nne;Madini ya Risasi katika Rangi*

Rangi yenye madini ya risasi ni hatari kwa afya ya binadamu kutokana na sumu na uchafuzi wa mazingira. Madini ya risasi yanapatikana katika rangi zinazotumika kupaka nje na ndani ya majengo, midoli, thamani na viwanja vya michezo.

*Tano;Dutu zinazoathiri mfumo wa homoni*

Tafiti kadhaa zimeonyesha uwepo wa dutu zinazoathiri mfumo wa homoni katika mazingira kupitia utupaji wa moja kwa moja wa dawa zilizoisha matumizi yake katika vyoo, madampo na taka za majumbani, au kupitia mifumo ya utoaji taka mwilini.

*Sita;Dawa zinazodumu katika mazingira kwa muda mrefu*

Dawa hizi huingia kwenye mazingira kupitia njia mbalimbali kama vile: mfumo ya maji taka, matumizi ya mbolea ya wanyama na kwenye majosho. Vilevile, uchafuzi wa mazingira unasabishwa na utupaji usiofaa wa dawa zisizotumika kutoka viwanda vya dawa.

*Saba;Viuatilifu Hatarishi*

Viuatilifu hatarishi ni viuatilifu ambavyo vimethibitika kusababisha madhara makubwa na ya muda mrefu kwa afya binadamu na mazingira kulingana na uchambuzi wa kimataifa ikiwemo shirika la Afya Duniani na Mikataba ya kimataifa ya mazingira. Viatilifu hivyo havitumiki katika nchi zilizoendelea bali zitumika kwa nchi zenye uchumi wa kati na zinazoendelea

# HABARI KATIKA PICHA




Mwenyekiti wa Bodi ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Prof. Esnati Chagu akimkabidhi Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Mussa Azzan Zungu Sheria na Kanuni za Mazingira.

*Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Mussa Azzan Zungu akisaini kitabu cha maombolezo kufuatia msiba wa kaka wa Naibu Katibu Mkuu Ofisi hiyo Balozi Joseph Sokoine jijini Dar es Salaam.*





*Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Azzan Zungu akikangalia vitalu vya miche ya miti katika kikundi cha mazingira cha Bwawani wilayani Sengerema mkoani Mwanza*


#Miaka56YaMuungano
AMANI
USALAMA
UMOJA
USHIRI-KIANO
MIAKA 56 YA MUUNGANO
BILA MTI MATUNDA TUNGEYASIKIA KWENYE BOMBA!
http://www.vpo.go.tz
FaceBook, Twitter, Instagram: ofisi_ya_makamu_wa_rais


MUUNGANO UMESAIDIA UDHIBITI WA UVUVI HARAMU BAHARINI
YES! UMOJA NI NGUVU, UTENGANO NI...
#Miaka56YaMuungano
http://www.vpo.go.tz
FaceBook, Twitter, Instagram: ofisi_ya_makamu_wa_rais

Limetolewa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Ofisi ya Makamu wa Rais
S.L.P. 2502, Dodoma, Tanzania
Simu: +255 266 235 2038
Nukushi: +255 266 235 0002
Baruapepe: ps@vpo.go.tz
Tovuti: www.vpo.go.tz
Facebook: ofisi ya makamu wa rais
Instagram: ofisi_ya_makamu_wa_rais
Twitter: @vpo_tanzania
Simu: +255 685 333 444